Serikali Wazi Hujivika Unyenyekevu

Hotuba iliyotolewa katika maadhimisho ya kwanza ya OGP
Rakesh Rajani, Twaweza, New York, 26 Septemba, 2012

Mawaziri, Marafiki, Mabibi na Mabwana:

Wakati tunaadhimisha mwaka mmoja wa Mpango wa kuendesha shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Governmnet Partnership* – OGP) tunajikuta tukiwa njiapanda. Kama ningekuwa mbahatishaji, ningesema kwamba uwezekano wa OGP kutimiza ahadi yake kamili ni moja kati ya tano.

Siyo kwamba hatujapiga hatua ya maana. Brazil, kwa mfano, hivi sasa ina sheria mpya yenye nguvu kuhusu uhuru wa habari ambayo imetokana na uanachama wake kwenye OGP. Ufilipino na Indonesia wanajadili mradi wa *checkmyschool* (*kagua shule yangu*) ili raia waweze kufahamu kama kweli fedha zinafika shuleni na kama wanafunzi wanasoma kweli au la. Nchini Tanzania, asasi ya kiraia kwa kushirikiana na Serikali watasambaza nakala milioni nne za kijitabu chenye lugha rahisi kitakacho waalika watoe maoni yao kuhusu namna gani Serikali inaweza kuwa wazi zaidi. Ulimwenguni kote misaada ya kigeni na uvunaji wa rasilimali ni masuala yanayozidi kuwekwa wazi zaidi. Na kuna mifano mingine mingi zaidi.

Kwa upande mmoja, endapo hata kama nchi kumi tu zinazoshiriki kwenye OGP zitafanikiwa walau theluthi moja ya yale ziliyodhamiria kufanya, OGP itakuwa imefanikiwa. Kwa asili, dhamira zilivyokaa ikiwa tu chache kati ya zilizowekwa zitafanikiwa basi zinaweza kuleta mabadiliko makubwa kwenye maisha ya mamilioni ya watu.

Pamoja na hayo, ukweli ni kwamba tunaweza kufanya vizuri zaidi kuliko matarajio ya chini.

Tulipokutana hapa mwaka mmoja uliopita, chini ya uongozi wa Rais Obama na Rais Rousseff, hatukusema kwamba hebu tufanye miradi muhimu chache. Tuliwekeana ahadi kubwa zaidi. Tuliahidi kuitikia msukumo wa watu kuhusu uhuru na utu ambao tuliushuhudia kupitia *Mageuzi ya Nchi za Kiarabu (Arab Spring)*, tuliyoona katika madai ya kuhakikisha rasilimali wananufaishi siyo wachache tu (*Occupy Wall Street*), sauti zinazodai huduma bora zaidi, kushirikishwa zaidi, kupata uhuru zaidi wa intaneti, na kukomesha rushwa.

Malengo ya msingi yalikuwa hasa kuleta mabadiliko kwenye uhusiano kati ya watawala na watawaliwa, kuhusu kuweka mfumo mpya ambapo Serikali hakika zinatumikia wananchi na kuweka mazingira ambayo kwayo watu wanapata ustawi.

Kwa jinsi mambo yalivyo, matumaini kwamba OGP itafikia dira hii ya kina zaidi ni madogo. Na kama jambo hilo litatokea, haitakuwa kwa sababu wakati haujafika au kwamba wananchi hawaitaki. Itakuwa kwa sababu sisi – hasa Serikali na asasi za kiraia ambao ni wanachama wa Kamati Tendaji ya OGP tutakuwa tumeshindwa kuonesha uongozi makini na hivyo kupoteza fursa.

Kazi yetu ni kuchukua hatua na kuweka mazingira ili uwezekano wa OGP kufanikiwa uongezeke.

Haitakuwa kazi rahisi. Kubadili utamaduni na mazoea yaliyojengeka kwa miaka mingi kila mahali ni jambo gumu; kubadili utamaduni za Serikali ni vigumu zaidi. Miaka mingi iliyopita, baba yangu alinipa ushauri. Aliniambia "Mwanangu, katika maisha huna budi kuepuka vitu vitatu: moto, dhoruba za bahari, na Serikali."

Ninaamini kwamba watu wengi duniani watakubaliana na ushauri huu. Hii ni kwa sababu uhusiano walio nao na Serikali ni ule wa taasisi kandamizi ambazo hazijali ustawi na matamanio yao, na mara nyingi huwakandamiza wananchi. Hapa tunamkumbuka Mohamed Bouazizi, yule mchuuzi wa matunda wa Tunisia, ambaye alikataa manyanyaso aliyofanyiwa na vikosi vya dola.

Si kila mwitikio wa wananchi unachukua sura kali kama ule wa Bwana Bouazizi. Lakini tusifanye kosa la kufikiri kwamba kwa vile hakuna kelele nyingi basi umma umeridhika. Katika nchi za Kaskazini na za Kusini kuna matamanio ya kina na fukuto la kutaka maisha bora, kuleta maendeleo kwa wote na si kwa kikundi kidogo tu cha watawala. Roho ya binadamu inaweza kughafirika kwa kiasi hicho tu pale inapotendewa udhalimu bila kikomo. Haiko wazi kama sisi tulio kwenye OGP tunailewa hilo vizuri, na kama tutaweza kuhimili changamoto iliyo mbele.

Hata pale ambapo Serikali na asasi za kiraia vinaridhia, kutimiza ahadi kamili ya dhamira zilizowekwa na OGP si rahisi; kutekeleza programu za maana ni jambo gumu sana. Nchini Kenya, tovuti ya wazi ya taarifa (*Open Data Portal*) inakusanya na kuweka hadharani taarifa za taasisi za umma, lakini ni wachache tu wanaoitumia. Nchini Tanzania, mradi wa kuwawezesha wananchi kutoa taarifa kuhusu vyanzo vya maji yaliyoharibika kupitia simu zao za mkononi, mradi ulioneshwa katika video ya uzinduzi wa OGP, mradi ambao taasisi yangu uliufadhili, umeshindwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu watu kukosa imani kwamba kutoa kwao taarifa kungeleta tofauti yoyote. Kwa ujumla, tukiwa wakweli kwa nafsi zetu, katika dhamira zaidi ya 300 za OGP, dalili za mafanikio ni kidogo sana. Hizi bado ni siku za mwanzo, lakini fursa yetu ya kujifunza na kutenda inazidi kutoweka kwa kasi.

Kipimo cha kweli cha ushirika wetu hakiko kwenye nchi ngapi zinatia saini kwenye Azimio la Serikali Wazi, bali ni dhamira ngapi zitatimizwa kikamilifu na kila nchi, na jinsi gani wananchi wataona mabadiliko ya maana katika maisha yao. Ndiyo maana *Mfumo Huru wa Tathmini* (*Independent Review Mechanism - IRM*) ya OGP, ambao utaanza kazi hivi karibuni, ni muhimu katika kuhakikisha mafanikio na kuwepo kwa uhalali wa OGP.

Kwa kutazama mbele, nini kitahitajika ili mchakato mzima uendelee kwenye nchi hizi? Hatuna budi kuvuta vipaji vyetu vyote, utayari na rasilimali. Katika vyote hivyo, ningependa kupendekeza kimoja kilicho muhimu sana.

Na kitu hicho ni unyenyekevu.

Unyenyekevu ni kukiri kwamba hatuna majibu kwa kila kitu. Ni Serikali kutojifanya inaweza kutatua matatizo yote yaliyopo, kutoa huduma kamilifu kabisa au kwamba inaweza kuleta uwajibikaji bora zaidi peke yake. Unyenyekevu ni kujenga utamaduni wa watu kutoa mawazo yao, kujenga udadisi wa kweli, na kuanzisha mifumo kivitendo kushughulikia mawazo hayo. Kwa sababu baadhi ya mawazo bora na ubunifu wenye manufaa makubwa hutoka nje ya fikra zilizozoeleka, kwa watu wasio wa kawaida.

Pili, unyenyekevu unakaribisha ukosoaji, hata pale unapoonekana kukosa uwiano na hauoneshi kuthamini kile tulichofanya. Ni wajibu wetu kuvuka vikwazo vya kelele na kutafuta ukweli katika yale wanayosema watu, na kuchukulia kama mrejesho muhimu, na kuutumia ili kujisahihisha. Zaidi, hata pale jambo hili lisipofikia matarajio hayo, hatuna budi kulinda ukosoaji kwa sababu haki ya kujieleza ni sehemu muhimu sana ya utu wetu. Ni kwa sababu hii kwamba ishara muhimu cha Serikali wazi kinaweza kuwa sheria bora inayolinda haki ya kupata taarifa na uhuru wa kujieleza – na utekelezaji wake wa maana.

Tatu, unyenyekevu ni kujenga njia mpya ya Serikali kuwasiliana na wananchi, njia ambayo si ya kutoa amri bali zaidi kuunda mazingira ambamo Serikali na wananchi kwa pamoja wanatatua matatizo ya jamii nzima. Ni kuheshimu haki za watu na weledi wao, kutumia teknolojia kwa njia za kina, kuwa tayari kuwajibika endapo mambo yatakwenda kombo na kukuza ubunifu. Ni kuwaomba raia kuwa wawajibikaji wenza kwa ajili ya hatima ya jamii nzima.

Serikali wazi yenye unyenyekevu ni serikali inayejiamini. Na pale inapozingatia ukweli na uwazi, inakuwa na nguvu kubwa kuliko nguvu yoyote ovu na inakuwa yenye ushawishi mkubwa zaidi kuliko ushawishi wa maneno marefu yasiyo na ukweli ndani yake.

Ninaamini kwamba wazo la serikali iliyo wazi ni muhimu sana, sambamba na mafanikio makubwa ya karne iliyopita, kama vile usawa kati ya wanaume na wanawake na usawa wa watu wa rangi zote; kwa hakika, kinachoongoza yote hayo ni msukumo wa ndani wa binadamu kutaka uhuru na utu. Ndiyo maana, licha ya wasiwasi wangu kuhusu majaliwa ya OGP, nina matumaini makubwa. Uwazi wa Serikali, uwazi wa mfumo tawala, ni muhimu mno kwa watu kiasi kwamba hatimaye kitaelekeza kupatikana kwa uwazi, kikisukumwa na vitendo vya mamilioni ya watu kila siku duniani kote. Changamoto iliyo mbele yetu, na fursa ya pekee, ni kujenga unyenyekevu na ufahamu wa kutufanya tuwe sehemu ya vuguvugu hili la mabadiliko.